

Ni kitu gani cha Kutegemea katika Uchunguzi wa Huduma za Ulinzi wa Watoto

Huduma za ulinzi wa watoto na uchunguzi wake zimekusudiwa kuhakikisha watoto wote wako salama, ikiwa amo na watoto wakimbizi na watoto wapya wenye wamefika. Hii mchoro inaeleza kitu kyenye kinatokea kawaida wakati wa uchunguzi wa CPS na kile jamaa za wakimbizi na jamaa za mupya zinaweza kutegemea.



START

Swali inaripotiwa



Mtu anawasiliana na Huduma za Ulinzi wa Watoto (CPS) kwa sababu ana wasiwasi kuhusu usalama au ustawi wa mtoto.

CPS Inachunguza Ripoti (Uchunguzi wa ku mwanzo / wakati ya mapokezi)



CPS inachunguza habari kusudi iamuwe:

- Je, hili jambo hili linakutanana na tafsiri ya kisheria ya unyanyasaji au kuzarauliwa kwa mtoto?
- Je, mtoto iko mu hatari ya pale pale?
- Kama majibu ni **hapana**, CPS haihusiki, na ripoti inafungwa.
- Kama majibu ni **ndiyo**, CPS itahusika na ile swali itachunguzwa zaidi.

Kukusanya Habari

CPS inaweza kukusanya habari kwa:

- Kuzungumuza na wazazi au walezi.
- Kuzungumuza na watoto (kwa njia yenye inalingana na miaka yao).
- Kuzungumuza na mtu mwenye alitoa ripoti na mtu mwingine yeyote mwenye anahusika na jamaa sawa vile Shirika ya makao ya mupya.
- Kutembelea kunyumba.
- Kupitia hii mawasiliano, mufanyakazi wa CPS anachunguza usalama wa mtoto, nguvu za jamaa, changamoto na musongo wa mawazo, na kupenda kujua ni msaada gani jamaa inahitaji.



CPS inawasiliana na jamaa

Kama CPS inakubali kesi kwa ajili ya uchunguzi, mufanyakazi wa CPS anaweza:

- Ita ku simu au tembelea jamaa.
- Eleza ni juu ya nini CPS inahusika.
- Uliza maswali kuhusu mtoto na jamaa.



Uamuzi wa Usalama

Kisha kuchunguza habari zote, CPS inaamua kama:

- Mtoto iko salama. Kama ni vile, kesi inaweza kufungwa.
- Msaada inahitajika. Kama ni vile, huduma zinaweza kutolewa.
- Kuko wasiwasi ya pale pale kuhusu usalama. Kama ni vile, mpango wa usalama inatengenezwa.
- Kutoshwa kwa mtoto haizoweyake kuwa na inafikiaka tu kama kuko hatari kubwa na hakuna njia ingine salama.



Mpango wa Usalama au Huduma (Kama Zinahitajika)

Kama CPS inaendelea kuhusika, inaweza:

- Kutengeneza mpango wa usalama pamoya na jamaa.
- Kutoa huduma za hiari au huduma za kuzuia matatizo.
- Kuiunganisha jamaa na huduma za msaada wa jamii..
- Mifano: Msaada wa malezi; huduma za ushauri au za afya ya akili; msaada wa makao, chakula, au malezi ya watoto; rasilimali za kiutamaduni au za kijamii.



Ufuatiliaji na Kufungwa kwa Kesi

CPS inaendelea kufuatilia pamoya na jamaa mpaka:

- Mtoto iko salama, na jamaa ya wakimbizi inapata msaada yenye wanahitaji.
- Kuhusika ya CPS inaisha na kesi inafungwa.



FINISH

